

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

614


MAARIFA YA JAMII

Muda: Saa 3

Mwaka: 2020

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenyé jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na C na maswali **mawili (2)** kutoka sehemu B.
3. Sehemu A ina jumla ya alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vikokotozi, simu za mikononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



2

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Eleza kwa kifupi sifa nne zinazotofautisha picha na ramani.
 2. Zifuatazo ni takwimu za kiwango cha mvua na halijoto ya eneo fulani. Soma takwimu hizo kisha jibu maswali yanayofuata.
- | Mwezi | J | F | M | A | M | J | J | A | S | O | N | D | Kwa mwaka |
|------------------------------|------|------|------|------|------|------|----|------|-----|------|------|------|-----------|
| Halijoto °S | 27 | 25 | 24.4 | 24.5 | 24.2 | 24.3 | 24 | 24.6 | 24 | 24.4 | 24.5 | 24.3 | |
| Kiwango cha Mvua (mm) | 40.8 | 69.0 | 150 | 232 | 205 | 118 | 65 | 84* | 195 | 226 | 150 | 50.8 | |
- (a) Eneo husika hupata kiasi gani cha mvua kwa mwaka?
 - (b) Kokotoa wastani wa kiwango cha mvua kwa mwaka cha eneo hili.
 - (c) Kwa kutoa sababu, eleza kwa kifupi aina ya tabia nchi inayowasikilishwa na takwimu hizi.
 - (d) Kwa kutoa sababu eleza kwa kifupi ni nchi gani ya kiafrika takwimu hizi zinaweza kuwa zilichukuliwa.
3. (a) Eleza sifa mbili za longitudo.
 - (b) Fafanua namna mbili ambavyo mistari ya longitudo hutumika.
 4. Kwa kifupi changanua umuhimu wa shughuli nne za kiuchumi zinazofanyika nchini Tanzania.
 5. Bainisha majanga manne ya asili kisha eleza kwa kifupi namna ambavyo athari zake zinaweza kupunguzwa.
 6. Kwa kifupi, elezea mabadiliko manne yanayoonesha mafanikio katika nchi za kiafrika baada ya kujipatia uhuru kutoka kwa wakoloni.
 7. Elezea kwa kifupi mbinu nne zilizotumiwa na nchi mbalimbali za kiafrika katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika.
 8. Fafanua kwa kifupi sababu nne zilizowafanya waingereza kupendelea zaidi mfumo wa utawala wa mlango wa nyuma katika makoloni yao.
 9. Elezea kwa kifupi sababu nne za kuundwa kwa Umoja wa Afrika.
 10. Ni kwa nini mataifa ya Ulaya yalivamia na kuligawa Bara la Afrika? Toa hoja nne.

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu swali **moja (1)** kutoka kila kipengele.

Kipengele I: Jiografia

11. Pendekesa njia tano endelevu zinazoweza kutumika kutunza mazingira.

12. Eleza vipengele muhimu vinavyowezesha ramani kutumika kwa usanisi.

Kipengele II: Historia

13. Eleza mabadiliko matano yaliyotokea katika maisha ya binadamu wakati wa zama za chuma.

14. Eleza mbinu tano ambazo wakoloni walizitumia katika kuimarisha utawala wao barani Afrika.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

15. Kwa kutumia hoja tano, tathmini udhaifu wa matumizi ya njia ya mhadhara kama mbinu ya kufundishia somo la Jiografia.

16. Ainisha njia tano zinazoweza kutumika kujipatia zana za kufundishia na kujifunzia somo la Historia.